

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA AROBAINI NA NNE**

**14 JUNI, 2022**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – TAREHE 14 JUNI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (*Monetary Policy Statement*) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Taarifa ya Ukaguzi wa Fedha za Msaada zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa kupitia Programu ya Kudhibiti na Kupambana na Majanga kuanzia Juni, 2020 hadi Aprili, 2022 (*Report on the Audit of Utilization of Funds issued under Catastrophe Containment and Relief Trust Facility from June, 2020 to April, 2022*).

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 387. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara za ndani za kilomita 10 katika Mji wa Karatu iliyotolewa na Rais wa Awamu ya Tano.

#### 388. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mikakati gani ya kupanua wigo wa miradi ya kuboresha barabara za mitaa ya Jimbo la Temeke kupitia DMDP.

#### 389. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya kuboresha na kupanua Vituo vya Afya vya Bungu, Magama na Mombo.

**390. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Zahanati ya Maisome kuwa Kituo cha Afya.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**391. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali inadaiwa fedha kiasi gani ilizokopa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kiasi gani cha madeni kimekipwa na kwa utaratibu gani.



**392. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za kukabiliana na athari mbalimbali za kiuchumi zinazotokana na hali ya kisiasa Duniani.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA  
BIASHARA:**



**393. MHESHIMIWA KHAMIS MBAROUK AMOUR  
(TUMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia Wamachinga ili waondokane na umachinga na kuongeza mapato ya nchi.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **394. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni kwa nini hadi sasa Wilaya ya Chake Chake ina Kituo kimoja cha Polisi.

## **WIZARA YA MADINI:**

### **395. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, hatua gani zimechukuliwa ili upatikanaji wa Baruti na Zebaki uwe rahisi na vibali kutolewa ngazi ya Kijiji kwa Wachimbaji wadogo.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

##### **SAA 10:00 ALASIRI**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA**  
**14 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**